# *Mambo Ambayo Kanisa La Foursquare Gospel Huamini…*

## Kanisa la Foursquare Gospel Huamini Katika:

1. **Maandiko Matakatifu**
   Tunaamini kwamba Biblia imepuliziwa pumzi ya Mungu. *(2 Timotheo 3:16,17)*

2. **Utatu Wa Mungu Wa Milele**
   Tunaamini kwamba Mungu ni Nafsi Tatu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. *(2 Wakorintho 13:14)*

3. **Kuanguka Kwa Mwanadamu**
   Tunaamini kwamba mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu; lakini alipoasi kwa hiari yake mwenyewe, alianguka kutoka katika hali ya ukamilifu. *(Warumi 5:12)*

4. **Mpango Wa Wokovu**
   Tunaamini kwamba Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi, na akatia sahihi msamaha wa wote wanaomwamini. *(Yohana 3:16; Warumi 5:8)*

5. **Wokovu Kwa Njia Ya Neema**
   Tunaamini kwamba sisi si wenye haki. Ni lazima tumjie Mungu kupitia kwa haki ya Kristo. *(Waefeso 2:8)*

### 6. Kutubu Na Kukubali

Tunaamini kwamba tukitubu halisi na kuku-bali Kristo kwa moyo wote, tunahesabiwa haki mbele za Mungu. *(1 Yohana 1:9)*

### 7. Kuzaliwa Upya

Tunaamini kwamba mabadiliko yanayofanyika moyoni na katika maisha ya mtu wakati wa wokovu, ni halisi kabisa. *(2 Wakorintho 5:17; Wagalatia 2:20)*

### 8. Maisha Ya Kikristo Ya Kila Siku

Tunaamini kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba tutakaswe kila siku, na kukua kila mara katika imani. *(Waebrania 6:1)*

### 9. Ubatizo Na Meza Ya Bwana

Tunaamini kwamba ubatizo kwa kuchovya ni ishara ya nje inayoonyesha tendo lilolofanyika ndani. *(Mathayo 28:19)* Tunaamini kufanya ukumbusho wa meza ya Bwana kwa kutumia mfano wa mkate na divai. *(1 Wakorintho 11:24,25)*

### 10. Ubatizo Wa Roho Mtakatifu

Tunaamini kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya kumtia nguvu anayeamini; na kwamba kuingia kwa Roho Mtakatifu ni kama ilivyokuwa katika siku za Biblia. *(Matendo 2:4)*

### 11. Maisha Ya Kujazwa Roho

Tunaamini kwamba Mungu anapenda tuenende kwa Roho kila siku. *(Waefeso 4:30-32)*

### 12. Karama Na Tunda La Roho

Tunaamini kwamba Roho Mtakatifu anazo karama za kumpa Mkristo; na kwamba tunapaswa kuonyesha tunda la roho kama dhihirisho la maisha yaliyojazwa Roho. *(1 Wakorintho 12:1-11; Wagalatia 5:22)*

### 13. Kuwa Na Kiasi

Tunaamini kwamba ujuzi wa Mkristo na mwenendo wake wa kila siku havipaswi kumwongoza katika hali ya kutokuwa na kiasi wala upole. *(Wafilipi 4:5)*

### 14. Uponyaji Wa Mungu
Tunaamini kwamba uponyaji wa Mungu husababishwa na nguvu za Kristo zinazomponya mgonjwa, anapojibu maombi ya imani. *(Yakobo 5:14-16)*

### 15. Kurudi Kwa Kristo
Tunaamini kwamba Kristo atarudi yeye mwenyewe mara ya pili, na kwamba kurudi kwake kumekaribia. *(1 Wathesalonike 4:16,17)*

### 16. Kushirikiana Na Kanisa
Tunaamini kwamba tunao wajibu mtakatifu kushirikiana na kanisa la Kristo linaloonekana. *(Matendo 16:5; Waebrania 10:25)*

### 17. Utawala Wa Serikali
Tunaamini kwamba watawala ni sharti waheshimiwe kila mara isipokuwa katika mambo yanayopinga mapenzi ya Mungo. *(Warumi 13:1-5)*

### 18. Hukumu Ya Mwisho
Tunaamini kwamba siku moja watu wote watasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu; ndipo watapokea uzima wa milele au mauti. *(2 Wakorintho 5:10)*

### 19. Mbiguni
Tunaamini kwamba mbinguni ni makao ya milele ya wote waaminio, Walozaliwa mara ya pili. *(Yohana 14:1-3; Ufunuo 7:15-17)*

### 20. Kuzimuni
Tunaamini kwamba kuzimuni ni mahali pa mateso ya milele, ambako wametayarishiwa wote wanaomkataa Kristo kama Mwokozi. *(Ufunuo 20:10,15)*

### 21. Uinjilisti
Tunaamini kwamba kuzihubiria roho za watu ni wajibu muhimu sana wa kanisa. *(Yakobo 5:20)*

### 22. Zaka Na Sadaka
Tunaamini Kwamba njia iliyowekwa na Mungu kwa ajili ya kusaidia na kueneza kazi yake ni kupitia kwa zaka na sadaka ya hiari. *(Malaki 3:10; 2 Wakorintho 9:7)*

Kuhusu Mambo ya Muhimu – Umoja

Kuhusu Mambo Yasiyo ya Muhimu – Uhuru

Katika Mambo Yote – Upendo

Je!Wajua…

Kanisa la Foursquare—ambalo linajulikana rasmi kama, International Church of the Foursquare Gospel—lilianzishwa huko Los Angeles, California, na Aimee Semple McPherson, Katika mwaka wa 1923.

Ushirika huu wa waaminio ulianzishwa wakati wa ufufuo wa miaka ya mwanzoni ya 1900. Lengo lake lilikuwa ni kuihubiri injili halisi ya ufufuo wa Kipentekoste, huku wakiepuka hali ya kutokuwa na kiasi (unafiki) na kupenda mali.

Mungu, kwa neema yake, ameturuhusu tukue kuanzia kwa ushirika mmoja tu hadi kuwa na makanisa yapatayo 1300 huko Amerika na Canada. Kadhalika, Kanisa la Foursquare limeanzishwa katika nchi zaidi ya 60 ulimwenguni kote. Idadi hiyo inaongezeka kwa haraka.

Hatuna haja ya kushindana wala kujilinganisha. Tunafurahia kila mwili wa waaminio ambao wanainua bendera ya Yesu Kristo iliyotapakaa damu. Kanisa la Foursquare ni mwanachama wa Shirika la Taifa la Makanisa Yanayoamini Mahubiri ya Injili (National Association of Evangelicals, yaani NAE), na kama Kanisa la Kipentekoste, limeshirikishwa katika Pentecostal Fellowship of North Amerika (PFNA).

Neno hili "Fourquare" hueleza huuma au kazi nne za Yesu Kristo kama Mwokozi *(Warumi 10:9)*, Abatizaye kwa Roho Mtakatifu *(Luka 3:16)*, Mponyaji *(1 Petro 2:24)* na Mfalme ajaye *(Matendo 1:11)*.

MISSIONS PRESS
© 2012
What the Foursquare Church Believes - Swahili